# IFAHAMU KAMPUNI YA AGREEN MIND LIMITED

@2023

YALIYOMO


1. UTANGULIZI ..... 3

KUHUSU SISI ..... 3

❖ Dira Yetu ..... 3

❖ Dhamira Yetu ..... 3

❖ Kauli mbiu ..... 3

2. MAADILI YA MSINGI ..... 4

3. HUDUMA ZETU KUU ..... 4

1. KILIMO-BIASHARA(Agribusiness) ..... 4

2. UKOMBOZI WA KIFIKRA ..... 4

3. VIWANDA ..... 4

4. MASOKO ..... 5

4. MBINU YETU ..... 5

5. UHALALI WA KAMPUNI ..... 5

6. UTAWALA WA USIMAMIZI ..... 6

7. MUUNDO WA KAMPUNI ..... 7

8. VIPAUMBELE VYA KAMPUNI KWA NDANI YA MIAKA 10 (2023-3033) ..... 8

MRADI WA PARACHICHI (Avocado Project) ..... 8

UKOMBOZI WA KIFIKRA (Mind-Set Transformation) ..... 8

WABIA WENYE TIJA (Strategic Partner) ..... 8

UHAMASISHAJI WA RASILIMALI (Resources Mobilization) ..... 8

MIKAKATI YA KIMASOKO (Strategic Marketing) ..... 8

UTAWALA BORA (Good Governance) ..... 9

9. NAMNA YA KUWA SEHEMU YA KAMPUNI ..... 9

10. WAJIBU WA KAMPUNI KWA MWEKEZAJI ..... 9

11. WAJIBU WA MWEKEZAJI KWA KAMPUNI ..... 10

12. KWA NINI UWEKEZE NA KAMPUNI YETU? ..... 10

12. MRADI WA PARACHICHI. ..... 11

Gharama za kuhudumia Hekari moja ..... 11

Mapato tarajiwa. ..... 12

14. Mawasiliano: ..... 13

15. SHUHUDA. ..... 14

# 1. UTANGULIZI

## KUHUSU SISI

**AGREEN MIND**, ni kampuni yenye lengo la kuifanya jamii ya kitanzania kuwa na maisha bora kupitia ukombozi wa kifikra na kilimo-Biashara kupitia zao la parachichi kwa kuzingatia mnyororo wa thamani (value chain).

Sanjari na hilo kampuni inahimiza wakulima kutumia mfumo wa mashamba ya pamoja ili kuongeza uzalishaji wenye tija na mafanikio kimasoko.

Kampuni hii imeanzishwa na vijana kama mfano wa kuigwa katika kuwakomboa vijana wengi wa kitanzania kwa kujiajiri wenyewe ili kuondokana na swala la ukosefu wa ajira na kupata kipato kupitia kilimo.

Kutokana na ongezeko la umasikini na ukosefu wa ajira, pamoja na changamoto za kifedha, Agreen Mind inatoa suluhisho kupitia uwekezaji katika kilimo kwa kufanya kazi na jamii inayotuzunguka wakiwepo vijana, waajiriwa, wafanyabiashara hadi wastaafu.

Jukumu kubwa tunalolifanya ni kuongoza na kutunza miradi ya mashamba ya pamoja ya kilimo kuanzia hatua ya utaftaji wa mashamba bora, kuyaandaa mashamba hayo kwa kupandwa parachichi hadi katika upatikanaji wa masoko ya uhakika.

Kampuni inaamini siku moja jamii itakuja kuondokana na maisha duni na kuwa na maisha bora kupitia Uwekezaji katika kilimo.

- **Dira Yetu**

  Jamii Endelevu Yenye Uchumi Unaokua.

- **Dhamira Yetu**

  Kuwekeza katika ukombozi wa kifikra na kilimo-Biashara pamoja na kuzingatia matumizi bora ya rasilimali kwa malengo ya kuleta maisha bora kwa jamii inayotuzunguka.

- **Kauli mbiu**

  *Kilimo Ni Ajira.*

## 2. MAADILI YA MSINGI

### 1. KAZI YA UJIMA (Teamwork)

Sisi ni timu tunayotambua uwezo na mchango wa kila mmoja katika kufanikisha maono ya kampuni.

### 2. UBUNIFU

Tunaweka bidii kukomboa jamii, na kutazama zaidi katika kukuza njia ya ubunifu ambayo huongozwa na vipaji, ubunifu na kujituma.

### 3. UADILIFU

Tunakuza tamaduni ya ukweli na uwazi kwa kila mmoja, na kujitolea kufanya kilicho sawa na haki. Tunafanya kwa uwazi ili kuthibitisha ukweli.

### 4. SHAUKU

Kukua kiubora, kuwapa furaha wateja wetu na kufurahia huduma zetu.

## 3. HUDUMA ZETU KUU

### 1. KILIMO-BIASHARA(Agribusiness)

Kampuni itahakikisha gharama za kufanikisha mradi zinakuwa ndogo ukilinganisha na faida itakayo patikana baada ya mavuno kwa zaidi ya miaka kumi (10) kwa kufanya sharing cost na cost of production analysisi pamoja na risk analysis ili kuleta tija kwa kutengeneza faida nzuri.

### 2. UKOMBOZI WA KIFIKRA

Kampuni inatoa semina, mikutano, midahalo, na mashauri yenye lengo la kuzibadilisha fikra za watu kuwa na mitizamo yenye kuleta tija katika kufanikisha maisha yanakuwa bora na kuondokana na ujinga na umaskini.

### 3. VIWANDA

Viwanda ni muhimu sana ili kusaidia kuchakata malighafi zitokanazo na zao la parachichi, kama sehemu ya kuibua ajira na utengemevu wa soko la ndani la zao la parachichi.

**4. MASOKO**

Kwa kufanya biashara ya mnyororo wa thamani kuanzia shambani hadi sokoni, kampuni itahakikisha bidhaa zinakuwa na ubora na zenye viwango vya kukidhi soko la ndani na nje ya nchi yetu pamoja na kufanya tafiti za kimasoko.

## 4. MBINU YETU

‘’Kukwepa umaskini kuna kila haja ya kuwa na pato huru la kifedha (financial freedom) kwa kila mmoja’’

Kwa Agreen Mind Company Limited, tunawakaribisha wawekezaji kuwekeza katika mradi wetu wa parachichi na kutoa huduma ya usimamizi kuanzia uzalishaji, uvunaji na kuyafikisha sokoni.

Uwepo wa ardhi yenye rutuba, mashine na wabobezi katika zao la parachichi tunakuhakikishia ubora mara zote.

Tunahakikisha usalama wa masoko ndani na nje ya nchi kwa ajili ya tunda la parachichi na kujali wawekezaji wetu kwa Bima ya mapato tarajiwa ya kwenye mradi wetu wa parachichi kwani usalama na faida ni lengo letu kubwa.

## 5. UHALALI WA KAMPUNI

Uhalali wa kampuni hii umetokana na ufanikishwaji wa mamlka za uasajili kama ilivyofafanuliwa kwenye jedwali

| Na. | Tasisi | Dhumuni | Namba ya usajili |
|---|---|---|---|
| 01 | Usajili wa kampuni | Mamlaka ya usajili wa biashara na lesseni | 152801440 |
| 02 | Mamlaka ya mapato Tanzania | Namba ya utambulisho wa mlipa kodi(TIN) | 152-801-440 |
| 03 | Manispaa ya Iringa | Lesseni ya Biashara | 171-0102-3645 |
| 04 | Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii(NSSF) | Utambulisho wa uchangiaji wa mfuko wa mafao ya wafanya kazi | 1041014 |

# 6. UTAWALA WA USIMAMIZI

Kampuni ya Agreen mind  Limited, inaongozwa na Bodi ya Wakurugenzi watano wakiongozwa na Bi. Emmanuela Mtafikolo Kaganda na Mr.Phinias Opanga wenye uzoefu mkubwa katika uongozi na usimamizi wa makampuni na miradi. Aidha Bodi kwa sasa inajumla ya wajumbe watano kama inavyooneshwa hapa kwenye Jedwali.

| **Na.** | **Majina** | **Wadhifa** | **Uraia** |
|---|---|---|---|
| 1 | Bi. Emmanuela Mtafikolo Kaganda | Mwenyekiti | Mtanzania |
| 2 | Mr. Phinias Samwel Opanga | Makamu Mwenyekiti | Mtanzania |
| 3 | Denis Paulo Ndamgoba | Katibu | Mtanzania |
| 4 | Joyce Loiruck Molle | Mjumbe | Mtanzania |
| 5 | Mr.George Kiegi Kasinga | Mjumbe | Mtanzania |

Kampuni vilevile inaongozwa na wafanyakazi 14, 8 wakiwa wanaume na 6 wakiwa wanawake. Kampuni pia ina wanahisa 20, 13 wakiwa wanaume na 7 wakiwa wanawake. Pia kampuni inajumla ya wawekezaji 15.

Kampuni pia ina jumla ya mabalozi 150 nchini kote, na kampuni imefanikiwa kuwafikia watu zaidi ya 400 kwa ajili ya ukombozi wa kifikra.

Kampuni hufanya kazi na watu Arobaini kwa siku.

## 7. MUUNDO WA KAMPUNI

Kampuni inaongozwa na muundo huu hapa katika kuratibu mambo na ufanyikaji wa maamuzi.



## 8. VIPAUMBELE VYA KAMPUNI KWA NDANI YA MIAKA 10 (2023-3033)

### MRADI WA PARACHICHI (Avocado Project)

Kwa sasa kampuni ina zaidi ya hekari 200 kwa ajili ya mradi wa kilimo cha parachichi, Mashamba yapo katika kijiji cha mapangali, Kata ya Imalutwa, Tarafa ya Mazombe, wilaya ya kilolo, Mkoa wa Iringa, ni kilomita 91 kutoka Iringa mjini na kilomita 45 kutoka barabara kuu ya kueleka Dar Es salaam. Ardhi hii ina udongo wenye rutuba, ipo karibu na mto Nyaga ambao hutililisha maji mwaka mzima. Kampuni itaendelea kuwaalika wadau mbalimbali ili kuweza kuungana na mradi huu ili ifikapo 2027 mradi huu uwe umeaza kuvunwa parachichi na kupeleka sokoni.

### UKOMBOZI WA KIFIKRA (Mind-Set Transformation)

Kilimo kimekuwa kikitazamwa kwenye jamii yetu kama adhabu au kama kazi ambayo mtu anaweza kujihusisha nayo endapo mtu akiwa ameshindwa katika mifumo mingine ya kimaisha hususani elimu, hivyo kampuni ya Agreen Mind imejikuta ni wenye deni katika jamii katika kuhakikisha tunakomboa fikra za vijana na jamii ya kitanzania kwa ujumla juu ya mtazamo wao kuhusu kilimo na kuwafanya waamini kuwa kilimo ni Ajira kama vile kauli mbiu yetu inavyosema. Tunawafikia vijana kupitia mafunzo mbalimbali kila wiki kwa njia ya semina, mikutano, shauri na mitandao ya kijamii.

### WABIA WENYE TIJA (Strategic Partner)

Kampuni pia inaendelea kutafuta wabia wenye tija katika kampuni yetu, mfano watu wenye mashamba mengine ya parachichi, au makampuni ya usambazaji wa miche, au hata watu binafsi wenye matunda ya parachichi mahali wanapoishi.

### UHAMASISHAJI WA RASILIMALI (Resources Mobilization)

Kampuni imeweka mkakati wa kuhakikisha haipotezi nafasi yoyote ya kukosa rasilimali ambazo zinaweza kutufikia kwa namna moja ama nyingine. Mfano mikopo kutoka kwenye Taasisi za kifedha, ruzuku au hata wafadhili.

### MIKAKATI YA KIMASOKO (Strategic Marketing)

Mradi huu unalengo la kuunganisha wakulima wa parachichi kwenye fursa, kwa kulima katika tija na uhakika wa soko.

**UTAWALA BORA (Good Governance)**

Kampuni inatekeleza sera za utawala bora kwa kuhakikisha kuwa wanaochaguliwa kuwa viongozi wa kitengo husika wana sifa za kielimu, uzoefu, maadili na moyo wa kupenda kufanya kazi pamoja na wenye mzigo wa kulikomboa Taifa letu.

## 9. NAMNA YA KUWA SEHEMU YA KAMPUNI

Kampuni bado inawakaribisha walengwa kati ya nafasi hizi ambazo zinapatikana katika kuendeleza ukuaji wa kampuni.

- Mwekezaji(Mkulima)

  Unaweza kulima pamoja na kampuni katika mashamba ya pamoja kwa kuingia mkataba na kampuni.
  Tembelea tovuti ya kampuni kisha jiandikishe kwenye mfumo wa kuomba uwe mmoja wa wawekezaji Kuanzia mwezi Januari hadi Septemba.

- Mbia (Partner).

  Unaweza kupata ushauri wa kitaalamu kupitia kampuni kwa kutembelea mashamba/ miti yako ya parachichi.
  Vilevile unaweza kuingia ubia na kampuni kwa kupata huduma ya ukombozi wa kifikra kwa kutembelea ofisi ya Mkurugenzi na kuona namna unavyoweza kuwa mdau.

- Balozi wa kampuni.

  Unaweza kujaza fomu ya kuwa balozi au kuandika barua ya kuomba nafasi hiyo ndani ya kampuni.

## 10. WAJIBU WA KAMPUNI KWA MWEKEZAJI

- Kufanya utafiti wa mashamba bora yanayofaa kwa kilimo cha parachichi,

Sifa hizo ni kama;

- Shamba lenye rutuba
- Shamba lisilo na migogoro
- Shamba lenye uwezekano wa miundo mbinu mizuri
- Shamba lenye urahisi wa upatikanaji wa maji
- Shamba lisilo na ukame

- Kuandaa bajeti ya gharama za mradi.

- Kuandaa mashamba, kupanda, na kusimamia kipindi chote cha miaka mitatu (3).
- Kusimamia shughuli za uvunaji katika kipindi cha miaka kumi (10).
- Kuhifadhi mazao kabla ya kwenda sokoni.
- Kufanya utafiti wa soko na kuuza matunda.
- Kufanya malipo ya wakati kwa mwekezaji.
- Kuandaa na kuratibu vikao vya wawekezaji.

## 11. WAJIBU WA MWEKEZAJI KWA KAMPUNI

- Kufanya malipo kwa wakati.
- Kuhudhuria vikao na matukio ya kimwaliko ihusuyo kampuni.
- Kutembelea mradi na kuona maendeleo.
- Kutoa mashauri ili kuleta tija katika mradi.
- Kuwa balozi wa kampuni.

## 12. KWA NINI UWEKEZE NA KAMPUNI YETU?

1. Uongozi bora, wenye tija na utaalamu wa kina.
2. Ni kampuni inayojikita zaidi na tafiti ili kufanya mradi wa kilimo kuwa ni wenye tija.
3. Uwepo wa ardhi yenye rutuba zaidi ya ekali 200 sehemu moja.
4. Uwepo wa ardhi isiyo na migogoro.
5. Miundombinu ya barabara inayofika hadi shambani.
6. Chanzo cha maji kwenye mradi ambapo itasaidia sana kwenye kilimo cha umwagiliaji.
7. Kampuni itajishughulisha na kukupelekea matunda sokoni kwa zaidi ya miaka kumi (10).
8. Ardhi ni mali ya mwekezaji na sio ya kukodi.
9. Kampuni ni ya kiubunifu katika mambo mengi inayofanya.
10. Usalama wa mradi wako ukiwekeza na kampuni.
11. Kuna Bima ya Mapato tarajiwa kwenye kila hekari utakayolima na kampuni.

## 12. **MRADI WA PARACHICHI.**

**Gharama za kuhudumia Hekari moja**

Unaweza kuanza na hekari moja katika ushiriki wako wa kulima kwenye mashamba ya pamoja.Aidha,ukilima nasi unaruhusiwa kulipa kwa mara moja gharama zote au kwa awamu tatu(Miaka mitatu) kama mchanganuo unavyoonesha kwenye jedwali:-

GHARAMA ZA MWAKA KWANZA

| NA. | MAELEKEZO | KIASI CHA GHARAMA (TSH) |
|---|---|---|
| 1 | Gharama Za Shamba Kwa Ekari 1 | 250,000 |
| 2 | Gharama Za Miche | 350,000 |
| 3 | Gharama za mbolea kupandia | 540,000 |
| 4 | Gharama za usafiri | 160,000 |
| 5 | Gharama mbolea kukuzia | 120,000 |
| 6 | Gharama za palizi | 300,000 |
| 7 | Gharama za kuchimba mashimo | 350,000 |
| 8 | Gharama za kusafirisha miche | 170,000 |
| 9 | Gharama za kupanda | 100,000 |
| 10 | Gharama kumwagilia miche shambani | 210,000 |
| 11 | Gharama viuwatilifu | 450,000 |
| 12 | Gharama za kukinga miche na jua | 300,000 |
| 13 | Utaalamu | 400,000 |
| | JUMLA NDOGO ( A) | **3,700,000** |

GHARAMA ZA MWAKA WA PILI

| NA. | MAELEKEZO | KIASI CHA GHARAMA (TSH) |
|---|---|---|
| 1 | Gharama za kupalilia | 200,000 |
| 2 | Gharama za viuwatilifu | 200,000 |
| 3 | Gharama za kumwagilia | 700,000 |
| 4 | Utaaalamu | 300,000 |
| | JUMLA NDOGO (B) | 1,400,000 |

GHARAMA ZA MWAKA WA TATU

| NA. | MAELEKEZO | KIASI CHA GHARAMA (TSH) |
|---|---|---|
| 1 | Gharama za viuwatilifu | 990,000 |
| 2 | Gharama za kumwagilia | 210,000 |
| 3 | Utaalamu | 300,000 |
| | JUMLA NDOGO (C) | 1,500,000 |
| | **JUMLA KUU (A+B+C)** | **6,600,000** |

Gharama hizi ni baada ya punguzo la kiasi cha fedha za kitanzania 2,000,000/=, hii inamaanisha kua gharama bila punguzo ni fedha za kitanzania 8,600,000/=
Punguzo hili ni kwa wale watakaowekena nasi kwa msimu wa mwaka 2023/2024 tu.

**Mapato tarajiwa.**

Kampuni inalima lakini pia inasimamia mashamba ya wengine ili kuleta dhana ya kulima mashamba ya pamoja. Hivyo basi katika mashamba ya wawekezaji kampuni imeweka utaratibu wa mgawanyo kwenye jedwali.

Kitaalamu na kihistoria mti wa parachichi huzaa matunda mfululizo zaidi ya miaka 30, lakini kampuni imeweka mapato tarajiwa kwa miaka 10 ya mwanzo kwa kila hekari moja. Kipindi cha miaka minne ya mwanzo ni matunzo.

Jendwali la mgawanyo wa mapato katika kila hekari

| MWAKA | JUMLA YA MAPATO TARAJIWA (TSH) | GAWIO LA MAPATO TARAJIWA KWA MWEKEZAJI 70% (TSH) | GAWIO LA MAPATO TARAJIWA KWA KAMPUNI 30%(TSH) |
|---|---|---|---|
| MWAKA WA 1 | 8,000,000 | 5,600,000 | 2,400,000 |
| MWAKA WA 2 | 14,000,000 | 9,800,000 | 4,200,000 |
| MWAKA WA 3 | 18,000,000 | 12,600,000 | 5,400,000 |
| MWAKA WA 4 | 20,000,000 | 14,000,000 | 6,000,000 |
| MWAKA WA 5 | 22,000,000 | 15,400,000 | 6,600,000 |
| MWAKA WA 6 | 22,000,000 | 15,400,000 | 6,600,000 |
| MWAKA WA 7 | 22,000,000 | 15,400,000 | 6,600,000 |
| MWAKA WA 8 | 22,000,000 | 15,400,000 | 6,600,000 |
| MWAKA WA 9 | 22,000,000 | 15,400,000 | 6,600,000 |
| MWAKA WA 10 | 22,000,000 | 15,400,000 | 6,600,000 |
| **JUMLA** | **192,000,000** | **134,400,000** | **57,600,000** |

## 14. Mawasiliano:

SIMU:

| Na. | Mhusika /Ofisi | Namba za simu | Barua pepe | Maudhui |
|---|---|---|---|---|
| 01 | Mkurugenzi Mtendaji | +255 629 456 941<br>+255 762 294 961<br>+255 744 182 388 | director@agreenmind.co.tz<br>deputydirector@agreenmind.co.tz | Masuala ya Kiutawala tu. |
| 02 | Meneja Mkuu | +255 756 485 578 | generalmanger@agreenmind.co.tz | Masuala yahusuyo Miradi na kuifahamu Kampuni |
| 03 | Ofisi ya Uhasibu | +255 766 470 503 | Finance@agreenmind.co.tz | Masuala ya husuyo fedha tu. |

Tovuti:www.agreenmind.co.tz

Iringa-Tanzania

Wilolesi,barabara ya Mwaibura.

Barua pepe:info@agreenmind.co.tz

## 15. SHUHUDA.



















DIRA YETU
DHIMA YETU






TUFIKE
Supreme



